# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# Taarifa kwa Vyombo vya Habari kuhusu Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2017

**Prof. Mussa Juma Assad**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

**10 Aprili, 2018**

**YALIYOMO**

UTANGULIZI ........................................................................... 1

SEHEMU YA KWANZA ........................................................................... 2

1. Tathmini ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Miaka Iliyopita na Hati za Ukaguzi kwa Mwaka 2016/17 ........................................................................... 2

SEHEMU YA PILI ........................................................................... 4

2. Matokeo ya Ukaguzi wa Serikali Kuu ........................................................................... 4

SEHEMU YA TATU ........................................................................... 12

3. Matokeo ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ........................................................................... 12

SEHEMU YA NNE ........................................................................... 15

4. Matokeo ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma ........................................................................... 15

SEHEMU YA TANO ........................................................................... 19

5. Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ........................................................................... 19

SEHEMU YA SITA ........................................................................... 21

6. Matokeo ya Ukaguzi Maalum ........................................................................... 21

SEHEMU YA SABA ........................................................................... 28

7. Ripoti ya Ujumla ya Ukaguzi wa Ufanisi ........................................................................... 28

## UTANGULIZI

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufanya kuwa wazima na wenye afya njema hadi siku hii ya kuwasilisha ripoti Bungeni. Pia ninamshukuru Mh. Rais kwa kuwasilisha ripoti za ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 Bungeni kwa wakati na hivyo kukidhi matakwa ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005.

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Zifuatazo ni ripoti za ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 zilizowasilishwa leo bungeni:

1. Ripoti ya Serikali Kuu;
2. Ripoti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
3. Ripoti ya Mashirika ya Umma;
4. Ripoti ya Miradi ya Maendeleo;
5. Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi; na
6. Ripoti 10 zinazohusu Ukaguzi wa Ufanisi katika sekta mbalimbali ambazo ni:

**Jedwali Na. 1: Ripoti 10 zinazohusu Ukaguzi wa Ufanisi katika Sekta mbalimbali**

| Na. | Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu; | | |
|---|---|---|---|
| 6.1 | Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Mwaka 2014 | 6.6 | Usimamizi wa Taka za Kieletroniki |
| 6.2 | Usimamizi wa Viuatilifu vya Kilimo | 6.7 | Usimamizi wa Maeneo Tengefu ya Ukanda wa Pwani |
| 6.3 | Usimamizi wa Ugawaji wa Viwanja | 6.8 | Usimamizi wa Urejeshwaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu |
| 6.4 | Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Maji Taka Maeneo ya Mijini | 6.9 | Maandalizi ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu |
| 6.5 | Utoaji wa Huduma za Kusaidia Viwanda Vidogo na vya Kati Nchini | 6.10 | Hali ya Uharibifu wa Ardhi na Misitu |

## SEHEMU YA KWANZA

### 1. Tathmini ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Miaka Iliyopita na Hati za Ukaguzi kwa Mwaka 2016/17

### 1.1 Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Miaka Iliyopita

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Ofisi yangu ilifanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa miaka iliyopita na kubaini kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuyafanyia kazi mapendekezo hayo.

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo hayo inaonesha kuwa kati ya mapendekezo 201 yaliyotolewa miaka iliyopita, mapendekezo 43 sawa na asilimia 21 yametekelezwa kikamilifu; mapendekezo 103 sawa na asilimia 52 utekelezaji wake unaendelea; na mapendekezo 55 sawa na asilimia 27 utekelezaji wake haujaanza. Mchanganuo wa utekelezaji umeainishwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa miaka iliyopita**

| Aina ya Ripoti | Idadi ya Mapendekezo | Utekelezaji umekamilika | | Utekelezaji unaendelea | | Utekelezaji haujaanza | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | % | | % | | % |
| **Mamlaka ya Serikali za Mitaa** | 68 | 03 | **5** | 34 | **50** | 31 | 45 |
| **Mashirika ya Umma** | 48 | 15 | **31** | 21 | **53** | 12 | 25 |
| **Serikali Kuu** | 85 | 25 | **29** | 51 | **60** | 9 | 10 |
| **Jumla** | **201** | **43** | **21** | **106** | **52** | **52** | **25** |
| ***Asilimia*** | ***100%*** | ***21%*** | | ***53%*** | | ***26%*** | |

### 1.2 Hati za Ukaguzi kwa Mwaka 2016/17

*Ndugu Waandishi wa Habari*,

Katika ukaguzi wa hesabu nilioufanya katika Serikali Kuu na taasisi zake, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2016/17 nimetoa jumla ya Hati 561 za ukaguzi. Kati ya hati hizo, Hati zinazoridhisha ni 502 sawa na asilimia 90, Hati zenye shaka ni 45 sawa na asilimia 8, Hati zisizoridhisha ni saba sawa na asilimia moja, na Hati Mbaya ni saba sawa na asilimia moja.

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi wa Hesabu kwa Mwaka 2016/17**

| Aina ya Ripoti | Jumla ya Hati | Hati Zinazoridhisha | | Hati Zenye Shaka | | Hati Zisizoridhisha | | Hati Mbaya | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | (%) | | (%) | | (%) | | (%) |
| Mamlaka ya Serikali za Mitaa | 185 | 166 | 90 | 16 | 9 | 3[1] | 1 | 0 | 0 |
| Mashirika ya Umma | 105 | 101 | 96 | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Serikali Kuu | 237 | 204 | 86 | 22 | 9 | 4 | 2 | 7[2] | 3 |
| *Jumla* | ***527*** | ***471*** | | ***42*** | | ***7*** | | ***7*** | |
| *Asilimia* | ***100%*** | ***90%*** | | ***8%*** | | ***1%*** | | ***1%*** | |

Aidha, katika ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na taasisi mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2016/17 nimetoa jumla ya Hati za Ukaguzi 742; ambapo Hati zinazoridhisha ni 697 sawa na asilimia 94, Hati zenye shaka ni 44 sawa na asilimia 5.9 na Hati isiyoridhisha ni moja; hati hii imetolewa kwa mradi wa maji (WSDP) unaotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Wilaya ya Makete.

[1] **Ripoti zenye hati zisizoridhisha ni:**
Halmashauri zilizopata hati zisizoridhisha ni Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani

[2] **Ripoti zenye hati mbaya ni:**
Alliance for Tanzania Farmers Party, Chama cha Kijamii, Chama cha Sauti ya Umma, National League for Democracy, Alliance for Tanzania Democratic Change, Tanzania Labour Party, Demokrasia Makini

## SEHEMU YA PILI

## 2. Matokeo ya Ukaguzi wa Serikali Kuu

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Ukaguzi wa Serikali Kuu na taasisi zake umebaini masuala mbalimbali ambayo ni pamoja na;

### 2.1 Mapato Yatokanayo na Kodi Zinazokusanywa na TRA

#### 2.1.1 Kesi za Muda Mrefu Katika Mamlaka za Rufaa za Kodi Trilioni 4.44

Katika mwaka wa fedha 2016/17 nilibaini kwamba, Mamlaka ya Mapato ina mashauri mengi ya kodi zilizokwama kwa muda mrefu katika Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa zenye kodi ya jumla ya shilingi trilioni 4.44. Taasisi hizi zina ufanisi mdogo unaochangiwa na upungufu wa makamu wenyeviti na wajumbe wa bodi zake, hivyo kupelekea kushindwa kufanyika kwa vikao vya kutosha kwa ajili ya kusikiliza na kuamua mashauri ya kodi.

**Jedwali Na. 4: Mashauri mbalimbali ya kodi yaliyokwama kwa muda mrefu**

| Mamlaka za Rufaa za kodi | Kiasi cha kodi | Asilimia |
|---|---|---|
| Bodi ya Rufaa za Kodi | Trilioni 3.57 | 80.2 |
| Baraza la Rufaa za Kodi | Bilioni 144.55 | 3.3 |
| Mahakama ya Rufaa | Bilioni 733.83 | 16.5 |
| **Jumla Kuu** | **Trilioni 4.44** | **100** |

#### 2.1.2 Mapungufu Katika Kushughulikia Pingamizi za Kodi (Tax Objections)

Katika mwaka 2016/17 nilibaini kuwa Mamlaka ya Mapato ina pingamizi za kodi zinazofikia Shilingi bilioni 738.61 ambazo bado hazijashughulikiwa.

Pia, Mamlaka ilipokea pingamizi za kodi zinazofikia Shilingi bilioni 296.09 bila kukusanya amana ya pingamizi au kupata kibali cha msamaha wa amana kutoka kwa Kamishna wa kodi kinyume na matakwa ya sheria ya kodi.

#### 2.1.3 Kukosekana kwa Uthibitisho wa Matumizi ya Mafuta Katika Shughuli za Migodi

Nilibaini kuwa malori 94 yaliyokuwa yamebeba mafuta lita milioni 3.147 yenye msamaha wa kodi ya Shilingi bilioni 2.08 kutoka Dar es Salaam kwenda migodi ya dhahabu minne (Buzwagi, Bulyanhulu, North Mara na Geita) kwa kipindi cha mwezi Julai, 2016 hadi Juni, 2017. Hata hivyo hapakuwepo nyaraka zinazothibitisha kuwa mafuta hayo yalipokelewa na makampuni hayo manne huko migodini. Kukosekana kwa

nyaraka hizo kunaashiria kwamba mafuta hayo hayakutumika kwa shughuli zilizokusudiwa za uchimbaji wa madini, hivyo kuisababishia Serikali hasara ya mapato.

**2.1.3.1 Mafuta Yaliyosamehewa Kodi ya Shilingi Bilioni 11.05 Yalitumiwa na Makampuni Yasiyostahili**

Ukaguzi ulibaini kuwa mafuta yaliyosamehewa kodi ya Shilingi bilioni 11.05 kwa ajili ya matumizi ya uchimbaji madini yalitumiwa na wakandarasi na watu wengine ambao sio wanufaika wa msahama huo katika kipindi cha mwezi Januari 2016 hadi Juni 2017. Hii ni kinyume na matakwa ya Agizo la Serikali Na. 480 lililotolewa tarehe 25 Oktoba, 2002.

**2.1.3.2 Mifumo Isiyoridhisha ya Udhibiti Mizigo Inayopitia Nchini Kwenda Nchi Nyingine**

Kadhalika, katika ukaguzi wa mafuta na mizigo inayopita nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine nilibaini lita milioni 26.14 za mafuta yenye kodi ya Shilingi bilioni 13.65 ambayo haikusafirishwa kwenda nchi zilizokusudiwa. Mapungufu haya yanamaanisha kuwa mizigo na mafuta haya yaliuzwa na kutumika ndani ya nchi bila kulipiwa kodi stahiki.

### 2.1.4 Udhaifu katika Ukadiriaji, Usimamizi na Ufuatiliaji wa Makusanyo ya Kodi yenye jumla ya Shilingi bilioni 271.65

Kwa mwaka wa fedha 2016/17, Mamlaka inadai kodi ya shilingi bilioni 262.29 kutoka kwa walipakodi mbalimbali. Kuwapo kwa madeni ya kodi kunasababishwa na mifumo na mikakati isiyoridhisha kwenye ukusanyaji wa madeni ya kodi hasa katika ofisi za mikoa. Aidha, nilibaini makadirio ya kodi yaliyokuwa pungufu kwa kiasi cha shilingi bilioni 9.363, yaliyosababishwa na mapitio na uchambuzi hafifu wa taarifa za walipakodi.

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

## 2.2 Tathmini ya Deni la Taifa

### 2.2.1 Ongezeko la Deni la Taifa

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017 Deni la Taifa lilikuwa ni shilingi trilioni 46.08 (2016: Sh. Trilioni 41.03) ikiwa ni ongezeko la shilingi trilioni 5.04 sawa na asilimia 12. Aidha, deni la ndani likiwa ni shilingi trilioni 13.33 na deni la nje shilingi trilioni 32.75.

### 2.2.2 Kutojumuishwa kwa Madeni Mengine ya Shilingi Trilion 4.58 Katika Deni la Taifa

Kiasi cha Shilingi trilioni 4.58 hakikujumuishwa katika deni la taifa kutokana na kutojumuishwa kwa madeni ya mifuko ya pensheni pamoja na dhamana ambazo masharti yake yalikiukwa.

### 2.3 Udhaifu Katika Ufuatiliaji wa Mikopo Inayotolewa na Mifuko Maalum ya Fedha za Serikali

Ukaguzi wa Mifuko Maalum ya Fedha za Serikali umebaini kuwa baadhi ya mifuko ina udhaifu katika ufuatiliaji wa mikopo iliyotolewa kwa vikundi mbalimbali. Hii inatokana kutokuwepo kwa jitihada za kufuatilia marejesho ya mikopo hiyo. Kwa mfano; Kiasi cha shilingi bilioni 1.14 kilikopeshwa na Mfuko wa ufadhili wa Pembejeo za Kilimo, na shilingi bilioni 1.08 zilikopeshwa na mfuko wa maendeleo ya Wanawake hata hivyo mikopo hiyo haijarejeshwa.

### 2.4 Kampuni za Madini Kutochangia Katika Mfuko wa Maendeleo ya Madini Shilingi Milioni 732.63

Katika ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Madini, nilibaini kuwa kiasi cha shilingi milioni 732.63 kilichotakiwa kutolewa na Mgodi wa Buzwagi Gold Mine unaomilikiwa na kampuni ya ACACIA Ltd hakikutolewa na Mgodi huu kinyume na ilivyokubalika katika Mkataba wa uzalishaji. Hivyo, kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na uchimbaji wa madini.

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

### 2.5 Ongezeko la Deni la Matibabu Nje ya Nchi Shilingi Bilioni 17.13

Ukaguzi wa gharama za matibabu nje ya nchi, ulibaini ongezeko kubwa la deni la gharama za matibabu nje ya nchi kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika hospitali za India kutoka kiasi cha Shilingi bilioni 28.60 kilichoripotiwa tarehe 30 Juni, 2017 hadi kiasi cha Shilingi bilioni 45.73 kufikia tarehe 31 Disemba, 2017. Ongezeko hili la asilimia 60.71 kwa kipindi kifupi, ni jambo linalohitaji Serikali kulifuatilia kwa makini ili kupunguza mzigo wa madeni na kuhakikisha kuwa hospitali husika zinalipwa kwa wakati.

### 2.6 Udhaifu Katika Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Vyama vya Siasa

Ukaguzi wa taarifa za fedha za vyama vya siasa ulibaini udhaifu katika uandaaji wa taarifa za fedha ikiwemo kutokuwepo kwa mfumo kubalifu wa uandaaji hesabu za vyama vya siasa. Aidha, kwa mwaka 2016/17 vyama vya siasa tisa (9) havikuwasilisha taarifa za fedha za kila mwaka wa ajili ya ukaguzi.

## 2.7 Mapungufu Katika Usimamizi wa Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2016/2017

Baadhi ya Mapungufu niliyoyabaini katika ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:

(i) Ubadhilifu wa shilingi milioni 332.86 katika Ubalozi wa Tanzania Nchini Maputo;

(ii) Hospitali za Sekretarieti za Mikoa tisa (9) zilipata hasara ya Shilingi milioni 343.62 iliyotokana na kukataliwa kwa madai yaliyowasilishwa NHIF baada ya kugundulika kuwa na dosari;

(iii) Malipo ya shilingi milioni 306.38 yalibainika kufanyika katika taasisi Sita (6) za Serikali Kuu ikiwa ni zaidi ya kiasi stahiki;

(iv) Taasisi 27 zilifanya malipo ya Shilingi bilioni 4.50 bila kuwa na nyaraka za kutosheleza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo;

## 2.8 Udhaifu Katika Usimamizi wa Mikataba na Manunuzi Katika Serikali Kuu

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017, nilibaini mapungufu kadhaa katika Taasisi za Serikali kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake wakati wa kufanya manunuzi kama ifuatavyo:

(i) Taasisi za Umma saba (7) zilibainika kufanya manunuzi ya Shilingi bilioni 2.99 bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kinyume na kifungu cha 35(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

(ii) Taasisi kumi na moja (11) zilinunua bidhaa na huduma za ujenzi zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.45 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila ya kuwa na mikataba kinyume na Kanuni ya 10(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

(iii) Taasisi kumi na nne (14) zilizokaguliwa zilinunua na kupokea bidhaa na huduma zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.68 bila ya kukaguliwa na kamati zinazohusika na ukaguzi na upokeaji wa bidhaa na huduma zilizonunuliwa, kinyume na matakwa Kanuni ya 244(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013. Hii inaweza kupelekea kupokea bidhaa zilizo chini ya kiwango.

(iv) Ukaguzi katika Taasisi za Serikali Kuu nane (8) umebaini manunuzi ya vifaa, kazi na huduma yenye thamani ya Shilingi bilioni 52.67 vilivyoagizwa na kulipiwa lakini havikupokelewa. Aidha, manunuzi hayo yanajumuisha malipo ya Shilingi bilioni 51.8 ambazo Serikali imelipia gharama za ndege aina ya Q400 Bombardier.

## 2.9 Udhaifu Katika Usimamizi wa Rasilimali Watu na Udhibiti wa Mishahara

Ukaguzi ulibaini madai ya watumishi ya jumla ya Shilingi bilioni 4.60 kwenye Serikali kuu ambayo hayakulipwa kwa watumishi hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha

unaoishia tarehe 30 Juni, 2017. Madeni hayo yanahusu upandishwaji vyeo, ajira mpya, stahiki za posho mbalimbali ikiwemo kukaimu madaraka na kujikimu.

**2.10 Kutorejeshwa kwa Mikopo ya Matrekta Shilingi bilioni 40.04**

Katika ukaguzi wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa, SUMA (JKT) nilibaini madai ya muda mrefu ya Shilingi bilioni 40.04 ambayo hayakukusanywa kutoka kwa wakulima waliokopeshwa matrekta na vifaa vya kilimo.

**2.11 Fedha Zilizotolewa Kwa Ajili ya Kulipa Madeni ya Miaka ya Nyuma**

Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 219.47 kilitolewa na Serikali kwa ajili ya kulipa madeni, ambapo, kiasi cha Shilingi bilioni 184.10 kilikuwa ni kwa ajili ya madeni ya matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 35 kwa ajili ya madeni ya matumizi ya maendeleo. Selikali imeendelea kulipa madeni yaliyohakikiwa ya Wazabuni, Wakandarasi, Watumishi na Watoa Huduma mbalimbali kwa kutegemea upatikanaji wa fedha. Ni maoni yangu kuwa, madeni ya miaka ya nyuma yaingizwe kwenye bajeti ya mwaka inayotarajiwa kulipwa ili kuepuka kuathiri utekelezaji wa bajeti.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

**2.12 Udhaifu Katika Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Vyama vya Siasa**

Ukaguzi wa taarifa za fedha za vyama vya siasa ulibaini udhaifu katika uandaaji wa taarifa za fedha ikiwemo kutokuwepo kwa mfumo kubalifu wa uandaaji hesabu za vyama vya siasa. Aidha, kwa mwaka 2016/17 vyama vya siasa tisa (9) havikuwasilisha taarifa za fedha za kila mwaka wa ajili ya ukaguzi.

**2.13 Mapungufu Katika Usimamizi wa Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2016/2017**

Baadhi ya Mapungufu niliyoyabaini katika ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:

(v) Ubadhilifu wa shilingi milioni 332.86 katika Ubalozi wa Tanzania Nchini Maputo;

(vi) Hospitali za Sekretarieti za Mikoa tisa (9) zilipata hasara ya Shilingi milioni 343.62 iliyotokana na kukataliwa kwa madai yaliyowasilishwa NHIF baada ya kugundulika kuwa na dosari;

(vii) Malipo ya shilingi milioni 306.38 yalibainika kufanyika katika taasisi Sita (6) za Serikali Kuu ikiwa ni zaidi ya kiasi stahiki;

**(viii)** Taasisi 27 zilifanya malipo ya Shilingi bilioni 4.50 bila kuwa na nyaraka za kutosheleza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo;

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

**2.14 Udhaifu Katika Usimamizi wa Mikataba na Manunuzi Katika Serikali Kuu**

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017, nilibaini mapungufu kadhaa katika Taasisi za Serikali kutozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake wakati wa kufanya manunuzi kama ifuatavyo:

(v) Taasisi za Umma saba (7) zilibainika kufanya manunuzi ya Shilingi bilioni 2.99 bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kinyume na kifungu cha 35(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

(vi) Taasisi kumi na moja (11) zilinunua bidhaa na huduma za ujenzi zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.45 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila ya kuwa na mikataba kinyume na Kanuni ya 10(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

(vii) Taasisi kumi na nne (14) zilizokaguliwa zilinunua na kupokea bidhaa na huduma zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.68 bila ya kukaguliwa na kamati zinazohusika na ukaguzi na upokeaji wa bidhaa na huduma zilizonunuliwa, kinyume na matakwa Kanuni ya 244(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013. Hii inaweza kupelekea kupokea bidhaa zilizo chini ya kiwango.

(viii) Ukaguzi katika Taasisi za Serikali Kuu nane (8) umebaini manunuzi ya vifaa, kazi na huduma yenye thamani ya Shilingi bilioni 52.67 vilivyoagizwa na kulipiwa lakini havikupokelewa.

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

**2.15 Udhaifu Katika Usimamizi wa Rasilimali Watu na Udhibiti wa Mishahara**

Ukaguzi ulibaini madai ya watumishi ya jumla ya Shilingi bilioni 4.60 kwenye Serikali kuu ambayo hayakulipwa kwa watumishi hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017. Madeni hayo yanahusu upandishwaji vyeo, ajira mpya, stahiki za posho mbalimbali ikiwemo kukaimu madaraka na kujikimu.

**2.16 Uchenjuaji Madini Bila Leseni**

Ukaguzi wa leseni za uchenjuaji madini kwa migodi iliyoko Mwanza, Kahama na Shinyanga, ulibaini kuwa mitambo nane iliyoko Mwanza, mitambo 25 Kahama na mitabo 51 Shinyanga ilikuwa ikiendeshwa bila ya kuwa na leseni hivyo kusababisha upotevu wa maduhuli ya Dola za Kimarekani 104,400, sawa na Shilingi milioni 231.66 za Kitanzania kwa mwaka.

## 2.17 Mapato yasiyotokana na Kodi Kutowasilishwa Mfuko Mkuu Shilingi bilioni 14.55

Ukaguzi ulibaini jumla ya Shilingi bilioni 14.55 zilikusanywa na balozi zetu nje ya nchi ikiwa ni mapato yasiyotokana na kodi kwa mwaka 2016/17, hata hivyo kiasi hicho cha fedha hakikupelekwa mfuko mkuu wa Serikali kinyume na matakwa ya Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2001; na kusababisha Serikali kushindwa kutumia fedha hizo. Vilevile, fedha hizo zaweza kutumika tofauti na ilivyokusudiwa

**Mapendekezo**

Nashauri Serikali:

i. Kuzingatia kikamilifu ushiriki wa Bodi ya Zabuni katika kuidhinisha manunuzi ili kuepuka manunuzi yasiyo kuwa na tija au mikataba isiyo tekelezeka kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 35 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011.

ii. Kufuatilia uletwaji wa vifaa vyote na pale inaposhindikana ihakikishe fedha zilizolipwa zinarejeshwa kutoka kwa Wazabuni na Wakandarasi, na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale walioshindwa kuleta vifaa na huduma.

iii. Kuchukua hatua muhimu ili kusimamia kwa ufanisi madeni na kuhakikisha yanalipwa kwa ukamilifu, hasa madeni ya matibabu ya ndani na nje ya nchi.

iv. Kuhakikisha kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa anakamilisha kuandaa mwongozo wa uandaaji wa hesabu za vyama ili kuwa na mwongozo wa uandaaji hesabu.

v. Kuimarisha utendaji wa mfumo mzima wa Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi katika kuendesha kesi za rufaa za kodi kwa kuhakikisha kuwa wakati wote nafasi za makamu wenyeviti na wajumbe wa Taasisi hizi zinajazwa kulingana na sheria husika.

vi. Kuongeza ufanisi katika kushughulikia kesi za pingamizi za kodi zilizowasilishwa na ili kutoa maamuzi juu ya kodi stahiki inayopaswa kulipwa kwa wakati.

vii. Kukusanya amana ya kodi stahiki kwa mujibu wa Sheria inayosimamia pingamizi za kodi.

viii. Kuhakikisha ukusanyaji wa kodi zote ambazo pingamizi zake zilikataliwa na ambazo maamuzi yake yametolewa na kuhitimishwa.

ix. Kupitia menejimenti ya SUMA kutumia dhamana zilizowekwa na wakopaji wakati wa kukopa ili kuhakikisha inakusanya madai yake yote ya shilingi bilioni 40 yaliyotokana na mikopo ya Matreka na zana nyingine za kilimo.

x. Kupitia Wizara ya Madini ihakikishe watu wote wanaojihusisha na mitambo ya kuchenjulia madini wanazingatia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake. Kushindwa kufanya hivyo ni kosa; na hatua za kisheria zichukuliwe kwa wakiukaji. Pamoja na hayo, ufuatiliaji wa hatua za kurejesha fedha ambazo hazijakusanywa ufanyike mara moja na Wizara husika.

xi. Kupitia menejimenti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashakiri kuhakikisha kuwa fedha zilizokusanywa zinahamishiwa Mfuko Mkuu kulingana na matakwa ya Kifungu cha 11 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 na kupunguza hatari ya fedha hizo kutumika kwa matumizi ambayo hayakukusudiwa ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za benki katika kutunza fedha hizo.

## SEHEMU YA TATU

### 3. Matokeo ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa umebaini masuala mbalimbali ambayo Serikali inapaswa kuyafanyia kazi ili kuboresha usimamizi wa rasilimali za Umma. Masuala hayo yameainishwa kwa kina katika ripoti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo nimeiwasilishwa kwako leo na muhtasari wake ni kama ulivyoainishwa katika sehemu hii.

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

### 3.1 Hali ya Fedha Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ukaguzi umebaini mapungufu kadhaa yanayohusu fedha zinazotolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida pamoja na zinazokusanywa kupitia vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hali hii inapelekea miradi mingi kutokukamilika na kuongezeka kwa madeni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 4 hapa chini:

**Jedwali Na. 5: Hali ya Fedha Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

| Na. | Upungufu uliojitokeza | Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | Kiasi (Sh.) Bilioni | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fedha za matumizi ya kawaida ambazo hazikutolewa | 146 | 581.52 | 15 |
| 2 | Fedha za matumizi ya maendeleo ambazo hazikutolewa | 167 | 532.21 | 51 |
| 3 | Fedha za Mapato ya ndani ambazo hazikukusanywa | 140 | 115.97 | 22 |

### 3.2 Mapato ya Shilingi Bilioni 3.53 Yaliyokusanywa na Wakala Kutowasilishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa 20 hazikupokea kiasi cha shilingi bilioni 3.53 kutoka kwa wakala ikiwa ni mapato ya ndani yaliyokusanywa na wakala mbalimbali. Hivyo, kuathiri utelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

### 3.3 Vitabu 379 vya Kukusanyia Mapato Havikuwasilishwa kwa Ukaguzi

Mamlaka za Serikali za Mitaa 21 hazikuwasilisha jumla ya vitabu 379 vya kukusanyia mapato licha ya kuombwa kufanya hivyo. Hivyo, sikuweza kuthibitisha kiasi cha mapato kilichokusanywa kupitia vitabu hivyo.

### 3.4 Kesi Dhidi ya Serikali za Mitaa Ambazo Zinaweza Kuathiri Utoaji Endelevu wa Huduma

Mamlaka za Serikali za Mitaa 116 zilikuwa na jumla ya kesi mahakamani zipatazo 1,111 zenye madai ya Shilingi bilioni 186.44 pamoja na gharama nyinginezo za kuendesha kesi. Kesi hizo zimetokana na kusitishwa kwa mikataba kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na wazabuni, kesi za watumishi na kesi zitokanazo na migogoro ya ardhi. Endapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zitashindwa katika kesi hizo, zitalazimika kulipa kiasi hicho cha fedha, hivyo kuathiri utoaji endelevu wa huduma.

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

### 3.5 Manunuzi Yaliyofanyika kwa Njia ya Nukuu za bei Badala ya Ushindani wa Kitaifa Shilingi Bilioni 1.19

Kwenye sampuli ya mikataba iliyokaguliwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, nilibaini mikataba mitatu (3) yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.19 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mbili (2), zilitumia nukuu za bei badala ya ushindani wa kitaifa kununua kazi zenye thamani inayozidi ukomo wa Shilingi Milioni 200 kama ilivyoainishwa katika jedwali la saba la Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

### 3.6 Kuchelewa Kukamilisha Miradi Shilingi Bilioni 1.65

Kulikuwa na ucheleweshaji katika utekelezaji na ukamilishaji wa miradi mitatu (3) yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.65 katika Halmashauri za Wilaya za Biharamulo, Karagwe na Mpwapwa.

### 3.7 Udhaifu Katika Usimamizi wa Rasilimali Watu na Udhibiti wa Mishahara

Ukaguzi ulibaini madai ya watumishi ya jumla ya shilingi bilioni 9.86 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 ambayo hayakulipwa kwa watumishi hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017. Madeni hayo yanahusu upandishwaji vyeo, ajira mpya, stahiki za posho mbalimbali ikiwemo kukaimu madaraka na kujikimu.

**Mapendekezo**

Ninaishauri Serikali:

i. Kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa fedha za ruzuku kwa matumizi ya kawaida na ya Maendeleo kwa wakati na kwa kiasi kilichoidhinishwa ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi.
ii. Kuboresha njia za ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuboresha usimamizi wa mifumo ya mapato.
iii. Kupitia Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhakikisha kuwa wanasheria wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatekeleza majukumu yao ipasavyo ikiwa ni pamoja na kusimamia kikamilifu uingiwaji wa mikataba na kuzishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa husika katika kufanya maamuzi sahihi.
iv. Kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafuata Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 katika usimamizi wa mikataba na manunuzi.
v. Kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madai ya watumishi kwa wakati na kuhakikisha kuwa uhakiki wa watumishi unafanyika mara kwa mara.

## SEHEMU YA NNE

## 4. Matokeo ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Ukaguzi wa Mashirika ya Umma ulibaini masuala mbalimbali ambayo Serikali inapaswa kuyafanyia kazi ili kuboresha usimamizi wa rasilimali za Umma. Baadhi ya masuala yaliyobainika katika uaguzi wa mashirika hayo ni pamoja na;

### 4.1 Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

Nimebaini vyeti vya ubora 3,911 vilivyotolewa na kampuni ya SGS vimeisha muda wake wa matumizi. Hata hivyo, TBS haikufanya uchunguzi wa suala hili kwa wanunuzi walioingiza bidhaa nchini. Pia, nimebaini kutokuwapo kwa maafisa wa TBS katika vituo zaidi ya 18 vya uingizaji bidhaa ili kuangalia ubora wa bidhaa zinazoingia nchini.

### 4.2 Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) Kutolipwa na Kampuni za Bima za Afya Shilingi Bilioni 1.86

Nimebaini kuwa kuna ankara za malipo za kiasi cha Shilingi bilioni 1.86 zilizokataliwa na kampuni za bima za afya kutokana na dosari kadhaa ikiwemo madai kwa ajili ya dawa ambazo hazikutolewa kwa wagonjwa.

### 4.3 Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)

#### 4.3.1 Uingizaji wa Bidhaa Zenye Thamani ya USD Milioni 1.94 kwa Kutumia Vibali vya Kughushi

Nimebaini kuwa waingizaji bidhaa kutoka nje, wameingiza bidhaa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1.94 kupitia vituo mbalimbali vya uingizaji bidhaa kwa kutumia vibali vya kughushi bila kubainika na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA). Hali hii inaashiria kuwapo kwa mianya katika taratibu za udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Chakula na Dawa.

### 4.4 Kampuni Hodhi ya Reli (RAHCO)

#### 4.4.1 Kutotekelezwa kwa Miradi Iliyofanyiwa Uchambuzi Yakinifu Wenye Gharama ya Shilingi Bilioni 20.1

RAHCO ilitumia zaidi ya Shilingi bilioni 20.1 kufanya upembuzi yakinifu kwa miradi iliyopangwa kutekelezwa ambayo ni (i) Arusha-Musoma, (ii) Mtwara-Songea-Mbambabay, (iii) Uvinza-Musongati-Mpanda-Karema, na (iv) Tabora-Kigoma-Kaliua-Mpanda. Hata hivyo, miradi hiyo haikutekelezwa kutokana na changamoto za kifedha licha ya kutumia gharama za awali za Shilingi bilioni 20.1 kufanya upembuzi huo.

### 4.4.2 TRA Kutowasilisha Ushuru wa Maendeleo ya Reli ya Shilingi Bilioni 194.31 kwa RAHCO

Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Mapato (TRA) ilikusanya Ushuru wa Maendeleo ya Reli wa Shilingi bilioni 194.31 bila kuwasilisha kiasi hicho RAHCO kulingana na matakwa ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2015.

## 4.5 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

### 4.5.1 Uwepo wa Dawa Zilizoisha Muda Wake Shilingi Bilioni 4.43

Ukaguzi ulibaini kuwa Bohari kuu ya dawa ina kiasi kikubwa cha dawa zilizoisha muda wake zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.43 ikiwa ni asilimia 2.4 zaidi ya kiwango kubalifu cha asilimia 1 ya gharama za mauzo. Kuendelea kuhifadhi dawa hizi kunaisababishia serikali gharama zisizo na tija.

## 4.6 Kutokuwapo kwa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma

Kwa mwaka huu wa ukaguzi, kulikuwa na Bodi za mashirika 20[3] ambazo zimemaliza muda wake; na hakuna Bodi mpya za kusimamia mashirika hayo zilizochaguliwa hadi ninakamilisha ukaguzi wangu mwezi Machi 2018. Baadhi ya taasisi zimekuwa zikiendelea na utendaji wa kazi bila ya Bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Kutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi na Wadhamini kunazorotesha shughuli za kiutendaji za mashirika hayo.

## 4.7 NSSF

### 4.7.1 Kutolewa kwa Mikopo Zaidi ya Kiasi cha Mkataba Shilingi Bilioni 6.18

NSSF iliingia Mikataba ya kutoa Mikopo kwa Taasisi nne kiasi cha Shilingi bilioni 60.69. Hata hivyo, nilibaini, NSSF ilizipatia taasisi hizo kiasi cha Shilingi bilioni 66.87 badala ya kiasi walichokubaliana, hivyo kiasi cha Shilingi bilioni 6.18 kilitolewa nje ya makubaliano ya mikataba. Kuna uwezekano wa Mfuko kutolipwa kiasi kilichotolewa nje ya makubaliano hivyo kupata hasara.

---

3 *Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA), Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TSLB), Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Kampuni Hodhi ya Kusimamia Ralisilimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO), Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA)*
*Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii (SSRA),Bodi ya Chai Tanzania (TBT), Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA), Baraza la Sanaa la Taifa (NAC), Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Wakala wa Uendelezaji wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA), Shirika Tija la Taifa (NIP), Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Bodi ya Bima ya Amana (DIB)*
*Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI).*

### 4.7.2 Tofauti ya Kiasi cha Uwekezaji Katika Dhamana za Serikali Shilingi Bilioni 1.05

Ukaguzi ulibaini tofauti ya Shilingi bilioni 1.05 katika rekodi za uwekezaji za NSSF dhidi ya rekodi za Benki Kuu. Uthibitisho wa Benki Kuu ya Tanzania ulibainisha kuwa Mfuko wa NSSF ulikuwa na uwekezaji wa thamani ya Shilingi bilioni 321.03 kinyume na taarifa za Mfuko huo za Shilingi bilioni 322.08.

## 4.8 Mapungufu ya Sheria Kumwezesha CAG Kukagua Uzalishaji na Mauzo ya Makampuni ya Madini, Mafuta na Gesi

Ukaguzi ulibaini kuwa sheria ya madini ya mwaka 2010 (kama ilivyorekebishwa 2017) na Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 hazijampa nguvu na mamlaka ya moja kwa moja Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata taarifa zinazohusiana na uzalishaji na mauzo ya rasilimali hizo kutoka kwenye Makampuni ya Madini, Mafuta na Gesi.

## 4.9 Mauzo ya Mali za Migodi Baada ya Muda wa Uchimbaji wa Madini kumalizika

Kifungu cha 22(a) cha Mfano wa Makubaliano ya Uzalishaji wa Pamoja wa Mafuta na Gesi (MPSA) kinataka mali zote zinazomilikiwa na mwekezaji na kutumika katika shughuli za uchimbaji mafuta na gesi kuwa mali za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) baada ya mkataba wa uzalishaji kuisha au kuvunjika au pale gharama zote za mali zinapokuwa zimerudishwa na mwekezaji. Hata hivyo, kwa upande wa Madini, Ukaguzi wa Mikataba ya Madini umebaini kuwa hakuna uhamishaji wa mali kwa Serikali pale ambapo gharama zote za mali zinapokuwa zimerudishwa na wawekezaji.

## 4.10 Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

### 4.10.1 Usimamizi Usioridhisha wa Mapato kutoka TICTS

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, hakuna usuluhishi na usimamizi madhubuti unaofanywa na Kitengo cha ufuatiliaji kuhusu mrahaba na tozo kwenye makontena yanayoenda nje ya nchi kupitia gati zinazosimamiwa na TICTS. Kutokuwapo kwa taarifa ya uwainishaji kunaifanya TPA kushindwa kuthibitisha kwa usahihi mapato yanayopatikana kupitia TICTS.

## 4.11 Chuo Kikuu Cha Dar es salaam

### 4.11.1 Malipo ya awali Bila Mkataba Dola za Marekani 161,381.95

Ukaguzi ulibaini kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kililipia Vifaa vya Spectrometer na Vifaa vya Maabara kutoka Chemetrix (Pty) vyenye thamani ya Dola za Kimarekani 86,102.95 na Dola za Kimarekani 75,279. Hata hivyo, malipo hayo yalifanyika kabla

mkataba rasmi kati ya pande mbili zilizousika. Chuo Kikuu kipo kwenye hatari ya kupoteza fedha hizo kutokana na kutokuwepo kwa mkataba.

**Mapendekezo:**

1. Bohari ya dawa inashauriwa kuweka mpango mkakati wa ununuzi na usambazaji wa dawa ili kuepuka kiwango kikubwa cha dawa kuisha muda wake kwa wakati mmoja. Pia, Bohari inapaswa kufuatilia mara kwa mara tarehe za kuisha kwa muda wa dawa ili kuhakikisha zinasambazwa na kugawiwa kwa muda unaopaswa.
2. Nashauri TBS ichunguze ikiwa hati 3,911 za ubora ziilizoisha muda wake zilitumika kuingiza bidhaa nchini na kuchukua hatua stahiki.
3. Nashauri RAHCO kutafuta namna ya kupata fedha za kutekeleza miradi husika ili kufikia malengo yaliyotazamiwa. Pia, siku zijazo RAHCO ihakikishe haifanyi upembuzi yakinifu kama fedha za utekelezaji wa miradi husika hazipo.
4. Ninashauri Mamlaka ya Mapato kuwasilisha kwa wakati kiasi chote cha makusanyo ya Ushuru wa Maendeleo ya Reli kwa RAHCO.
5. Chuo Kikuu kinatakiwa kuhakikisha kwamba mikataba yote imewekwa saini kabla malipo kufanyika na kuhakikisha bidhaa zilizolipiwa zina letwa na mzabuni.
6. Tunashauri serikali iteue Bodi za Wakurugenzi na wadhamini kwa wakati pindi zinapomaliza muda wake. Pia Bodi zipitie na kupitisha taarifa za hesabu kwa muda muafaka ili kuwezesha mchakato wa ukaguzi kuendelea na kukamilika kwa wakati.

## SEHEMU YA TANO

## 5. Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo umebaini masuala mbalimbali ambayo Serikali inapaswa kuyafanyia kazi ili kuboresha usimamizi wa rasilimali za Umma. Masuala hayo ni pamoja na;

### 5.1 Kutolipwa Fidia ya Shilingi Bilioni 11.87 kwa Watu Walioathiriwa na Miradi

Nimeibaini kuwa watu walioathiriwa na utekelezaji wa miradi mitatu; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II), Programu ya Msaada wa Sekta ya Usafiri (TSSP) na Mradi wa Barabara ya Arusha-Taveta/Holili-Voi hawajalipwa fidia ya jumla ya Shilingi bilioni 11.87.

### 5.2 Kutolipwa kwa Gharama za Uchangiaji Kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na "Global Fund" Shilingi bilioni 61.4

Ukaguzi umebaini kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu (Global Fund) hawakuchangia jumla ya Shilingi bilioni 61.4; Hii ikiwa ni asilimia 5.6 ya jumla ya gharama zote za uhifadhi na usambazaji kwenda Bohari ya Dawa (MSD) kwa ajili ya gharama za uhifadhi na usambazaji wa dawa na vifaa-tiba kama inavyoelekezwa na mkataba baina yao.

### 5.3 Malipo ya Riba Yatokanayo na Kucheleweshwa kwa Malipo ya Wakandarasi Shilingi Bilioni 3.9

Nilibaini kuwa jumla ya Shilingi bilioni 3.88 zililipwa kama riba kutokana na kutolipa madai ya wakandarasi kwa wakati yaliyohusisha miradi ya Programu ya Msaada katika Sekta ya Barabara Awamu ya Kwanza (RSSP I), RSSP II na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji awamu ya pili (WSDP II). Ucheleweshwaji wa malipo ya wakandarasi ulitokana na Hazina kutopeleka fedha za miradi kwa wakati.

## 5.4 Fedha za Ushuru wa Mafuta na Usafirishaji Zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania Shilingi Bilioni 14.8 Hazikupelekwa Kwenye Akaunti ya Mfuko wa Barabara

Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya kiasi cha Shilingi bilioni 755.68 kama ushuru wa mafuta na usafirishaji, hata hivyo Mamlaka ilihamisha kiasi cha Shilingi bilioni 740.85 kwenda kwenye akaunti ya Mfuko wa Barabara hivyo kiasi cha Shilingi bilioni 14.82 hakikupelekwa.

**Mapendekezo**

Ninashauri Serikali:

i. Kutoa fidia mapema kwa watu waliothibitika kuwa wameathiriwa na miradi.

ii. Kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mfuko wa Kimataifa wa Malaria, UKIMWI na Kifua kikuu walipe kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 61.4 kama sehemu ya kuchangia gharama za Bohari ya Dawa. Aidha taratibu zifanyike ili kutambua deni la nyuma na kuweza kuwa na makubaliano ya jinsi ya kulilipa.

iii. Kuhakikisha kuwa madai ya wakandarasi ya yanalipwa kwa wakati ili kuepuka gharama zitokanazo na ucheleweshaji wa malipo. Aidha watekeleza miradi wanashauriwa kuyapa kipaumbele na kuyawasilisha Hazina madai ya wakandarasi ambayo yana uwezekano wa kuwa na adhabu ya ucheleweshaji endapo hayatalipwa kwa wakati.

iv. Kupitia Menejimenti ya Mfuko wa Barabara inatakiwa iwasiliane na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) warejeshewe kiasi cha Shilingi za Kitanzini bilioni 14.8 kinachotokana na makusanyo ya ushuru wa mafuta na usafirishaji.

## SEHEMU YA SITA

## 6. Matokeo ya Ukaguzi Maalum

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

### 6.1 Ukaguzi Maalum Uliofanyika Katika Idara ya Uhamiaji

### 6.1.1 Matumizi Mabaya ya Mapato Yanayofikia Shilingi Milioni 205.46

Ukaguzi maalum ulibaini udhibiti dhaifu wa ndani kwenye makusanyo ya mapato katika Idara ya Uhamiaji. Hali hii ilipelekea upotevu wa mapato ya jumla ya Shilingi milioni 205.46 kutokana na kutopelekwa benki.

### 6.1.2 Gharama ya Manunuzi ya Shamba Iliyolipwa zaidi kwa Kiasi cha Shilingi Milioni 132.36

Idara ya Uhamiaji, kupitia Bodi ya zabuni ya Wizara ya Mambo ya Ndani, ilinunua Shamba Na. 622 lililopo eneo la Kasumulu, mkoani Mbeya kwa Shilingi milioni 340. Ukaguzi ulibaini kuwa shamba hilo lina ukubwa wa hekta 1.47225 kinyume na taarifa ya uthamini iliyoonesha ukubwa wa hekta 2.4108 hivyo kusababisha ongezeko la gharama kwa Shilingi milioni 132.36 ambazo hazikustahili kulipwa.

### 6.2 Ukaguzi Maalum Uliofanyika Katika Soko la Mwanjelwa

### 6.2.1 Hasara ya fedha za Umma iliyobainika katika ukaguzi maalum wa Soko la Mwanjelwa

i. Ongezeko la gharama za ujenzi baada ya mkataba ulioingiwa na mkandarasi Tanzania Building Works Ltd kuvunjwa Shilingi bilioni 5.81
ii. Hasara iliyosababishwa na kutomshirikisha Mshauri Mwelekezi katika mchakato wa kumpata mkandarasi wa pili Shilingi milioni 682.79
iii. Malipo ya awali yalilipwa kwa Tanzania Building Works Ltd zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa na mkataba Shilingi bilioni 1
iv. Madai ya dhamana ya utekelezaji Na: 109/2012 dhidi ya M/S Jubilee Insurance Company of Tanzania Ltd ambayo hayakulipwa Shilingi bilioni 1.06
v. Tozo za ucheleweshaji kazi ambayo haijalipwa na Tanzania Building Works Ltd kwa H/Jiji la Mbeya kwa kuchelewa kumaliza kazi kwa wakati Shilingi bilioni 1.03
vi. Hasara ambayo Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilipata kwa kuchukua mkopo benki ya CRDB badala ya NSSF Shilingi bilioni 5.13
vii. H/Jiji la Mbeya kushindwa kukusanya kodi ya pango Shilingi bilioni 1.22 baada ya wapangaji kushindwa kufanya biashara katika soko hilo kutokana

na bei za juu za kodi ya pango ikilinganishwa na zile za soko katika eneo hilo.

viii. Hasara iliyotokana na kuchukua mkopo kutoka Benki ya CRDB kabla shughuli za ujenzi hazijaanza rasmi Shilingi bilioni 3.36

ix. Malipo kwa Mkandarasi M/S Tanzania Building Works Ltd yanayozidi kazi alizofanya Shilingi bilioni 1.14

x. Mabadiliko na nyongeza za kazi zilizotokana na uzembe na kukosekana weledi katika usanifu wa Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mwanjelwa Shilingi bilioni 3.16

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

**6.3 Ukaguzi Maalum wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT)**

Ukaguzi huu maalum katika chama cha waalimu Tanzania ulijikita katika tuhuma dhidi ya Uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania zinazohusu ubadhirifu wa fedha na mali za Chama. Ukaguzi huo ulibaini yafuatayo:

**6.3.1 Malipo Yaliyofanyika Bila Viambatisho vya Kutosha Shilingi Bilioni 10.27**

Ukaguzi wangu umebaini malipo ya matumizi mbalimbali ya Ofisi yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.27 kukosa vielelezo vya uthibitisho wa matumizi hayo kinyume na matakwa ya Kanuni za Fedha Toleo la pili la Mwaka 2011(b) (v). Hali hii ilipelekea kushindwa kujua uhalali na usahihi wa malipo hayo.

**6.3.2 Malipo Yasiyoidhinishwa Shilingi Bilioni 3.28**

Uchunguzi umebaini kuwa malipo yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.28 yalifanyika bila kuidhinishwa na Katibu Mkuu na Mweka Hazina wa Chama cha Walimu kwa kipindi kinachoanzia 2011 mpaka 2016. Hii ni kinyume na kifungu katika nyongeza ya pili (b)(v) ya kanuni za fedha za mwaka 2011 ambayo inahitaji viambatisho vyote vilivyoidhinishwa viambatishwe kwenye hati za malipo husika.

**6.3.3 Usimamizi Usiofaa wa Miradi ya Uwekezaji Katika Benki ya Walimu (MCBL) na Mwalimu House**

Tathmini iliyofanyika kuhusu umiliki wa Benki ya Walimu (MCBL) na Mwalimu House umebaini mapungufu yafuatayo:

(i) Hakuna nyaraka zinazoonesha umiliki wa moja kwa moja wa Chama cha Waalimu juu ya Miradi yake ya Uwekezaji.

(ii) Hakuna nyaraka zinazoonesha mtiririko wa mapato yatokanayo na miradi ya uwekezaji iliyofanywa na Chama cha Walimu tangu kianzishwe.

(iii) Chama cha Waalimu kilinunua hisa 8,000,000 sawa na asilimia 12.94 ya umiliki katika kampuni yake ya MCBL, hivyo kutokuwa na maamuzi ndani ya kampuni waliyoianzisha wao wenyewe.

(iv) Kampuni ya Mwalimu House imeanzishwa na CWT na kupelekwa kwa kampuni ya TDCL kwa ajili ya usimamizi bila kuwa na mkataba ambao unaonyesha jinsi CWT na wanachama wake watakavyofaidika na mapato yatokanayo na jengo hilo.

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

### 6.4 Ukaguzi Maalum Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

#### 6.4.1 Ubadhilifu wa Fedha Uliotokana na Ukodishaji wa Jengo la Ofisi Shilingi Milioni 402.21

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa menejimenti ya NIDA kwa kushirikiana na mmiliki wa jengo (kampuni ya BMTL), na kampuni ya Gotham International Limited (GIL) walishiriki katika kufanya ubadhilifu wa fedha za Serikali wa kiasi cha Shilingi Milioni 402.21 kupitia ukodishaji wa jengo kwa ajili ya matumizi ya ofisi. Ubadhilifu huu ulitokana na kuongeza ukubwa wa eneo kwa mita za mraba ($m^2$) 254.1 hewa kutoka mita za mraba ($m^2$) 1,946.9 hadi mita za mraba ($m^2$) 2,201 hivyo kusababisha ongezeko la kodi ya pango kwa kiasi cha shilingi milioni 402.21.

#### 6.4.2 Mamlaka Ilipata Hasara ya Shilingi Milioni 167.44 kwa Kutumia Viwango vya Benki za Biashara Badala ya Viwango vya Benki Kuu Kinyume na Mkataba

Ukaguzi wangu umebaini malipo yaliyofanywa katika Shilingi za kitanzania kwa viwango vya kubadilishana vilivyoonyeshwa na Mabenki ya Biashara badala ya viwango vya ubadilishaji vilivyoainishwa na kutolewa na Benki Kuu ya Tanzania na hivyo kuisababishia Mamlaka hasara ya Shilingi milioni 167.44.

#### 6.4.3 Malipo ya Ushauri Elekezi Kufanyika Mara Mbili na Kusababisha Hasara ya Shilingi Milioni 899.93

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Mamlaka ya vitambulisho (NIDA) iliingia mkataba na kampuni mbili tofauti (Gotham International Limited na M-S Law Partners) katika kutoa Ushauri Elekezi wa Kisheria hivyo kufanya malipo mara mbili kwa kazi moja na kuisababishia Mamlaka hasara ya jumla ya Dola za Marekani 551,500 sawa na Shilingi milioni 899.93.

### 6.5 Ukaguzi Maalum wa Fedha za Shirikisho la Serikali za Mitaa (ALAT)

Ukaguzi wangu wa ALAT ulibaini yafuatayo;

(i) Menejimenti ya ALAT ilitumia fedha kiasi cha Shilingi milioni 284.59 kwa matumizi ya kawaida bila kupata kibali kutoka Mkutano Mkuu wa Mwaka.

(ii) Jumla ya Shilingi bilioni 3.76 zililipwa kwa shughuli mbalimbali bila kuwa na viambatisho stahiki na pia kupitia nyaraka na miamala ya benki iliyogushiwa.

(iii) Fedha za ALAT ziliwekwa kwenye akaunti ya kampuni binafsi (M/S Vision Investment) kiasi cha shilingi milioni 150 bila kibali kutoka kwa menejimenti.

(iv) Menejimenti ya ALAT ilishindwa kuwasilisha viambatanisho vya malipo yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.56.

(v) Aidha, nilibaini udanganyifu wa malipo ya Shilingi milioni 76.66 na makusanyo ya mapato ambayo hayakupelekwa benki ya kiasi cha Shilingi milioni 14.33.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

### 6.6 Ukaguzi Maalum juu ya Ujenzi wa Mtandao wa Usambazaji Umeme kwa Ajili ya Mradi wa Mtwara (MEP)

Ukaguzi huu maalum ulikua na lengo la kuhakiki uhalali na usahihi wa gharama za kurejesha zilizotumika wakati wa ujenzi wa mtandao wa usambazaji umeme Mtwara (MEP).

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Serikali inatakiwa kurudishiwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 8.42 kutoka kwa kampuni ya Wentworth Gas Limited na kampuni yake ndogo M/S Umoja Light Company Limited ikiwa ni gharama ambazo hazijakidhi matakwa ya mkataba yaliyopo katika mikataba ya Tariff Equalization Fund (TEF) na Masasi Interconnection Construction and Reimbursement Agreement (MICRA).

### 6.7 Ukaguzi Maalum Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)

#### 6.7.1 Vifaa vya Shilingi Bilioni 34.4 Vyenye Msamaha wa Kodi Kutotumika Kwenye Mradi Kusudiwa

Ukaguzi umebaini kuwa, vifaa vyenye thamani ya Shilingi bilioni 34.4 vilivyoingizwa nchini na kampuni ya Star Media na kupata msamaha wa kodi havikufungwa kwa ajili ya matumizi ya mradi licha ya kuoneshwa kwenye orodha ya mali kwamba vimefungwa.

#### 6.7.2 Kampuni ya Star Media Kutoza Uchakavu wa USD Milioni 30.11 isivyo halali

Kampuni ya Star Media imekuwa ikitengeneza hasara kwa zaidi ya miaka 7 mfululizo iliyochangiwa na kutoza uchakavu kinyume na utaratibu kwenye ving'amuzi

vilivyouzwa kwa wateja. Hii imepelekea jumla ya Dola za Marekani milioni 30.11 kutozwa kutoka kwenye mapato kwa kipindi cha miaka 6 kuanzia 2010 mpaka 2015 hivyo kuikosesha TBC faida na gawio.

#### 6.7.3 Kampuni ya Star Media Kutochangia Gharama ya Mtaji USD. 650,000

Kifungu cha 1.4 na 1.5 cha Randama ya Makubaliano kati ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Star Times kinaainisha mtaji wa ushirikiano kuwa ni Dola za Marekani milioni 1 utakaotokana na hisa 10,000 zenye thamani ya Dola za Marekani 100 kila moja. Mgawanyo wa mtaji ni asilimia 35 kwa TBC sawa na Dola za Marekani 350,000 na asilimia 65 kwa Star Times sawa na Dola za Marekani 650,000. Hata hivyo, nimebaini kuwa Star Times haikuwahi kutoa fedha za mtaji kama sehemu yake ya umiliki wa Star Media kinyume na makubaliano hayo.

#### 6.7.4 Mfuko wa Hisani wa Kuendeleza Sekta ya Korosho (CIDTF)

Nimebaini kutokuwasilishwa kwa tani 837 za mbolea ya Salfa zenye thamani ya Shilingi milioni 803.52 zitokanazo na mkataba ulioingiwa na kampuni ya Hammers Incorporation Ltd kwa ajili ya kusambaza tani 3,000 za Salfa. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji wa mkataba, mzabuni alisambaza jumla ya mifuko yenye uzito wa tani 2,163 na kuacha kuleta mifuko yenye uzito wa tani 837.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

### 7.1 Ubia wa Uendeshaji kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Kampuni ya Intra Energy Tanzania Limited(IETL)

#### 7.1.1 Matumizi Yasiyo Halisi Katika Utafutaji wa Madini Kiasi cha Shilingi Milioni 880.7 Yaliingizwa Katika Taarifa za Fedha za TANCOAL ENERGY LTD

Uchambuzi wa taarifa za fedha pamoja na Ripoti ya Utafutaji wa Madini ulibainisha gharama za utafutaji wa madini za Shilingi bilioni 6.58; ambapo, kiasi cha Shilingi milioni 880.7 kati ya hizo kilijumuishwa isivyostahili.

Gharama hizi ziliainishwa katika taarifa za fedha kwa miaka minne kuanzia mwaka 2013 hadi 2016 isivyostahili, kwani utafiti wa madini uliisha mwaka 2012. Kuingizwa kwa gharama za aina hiyo katika taarifa za kifedha kumepunguza faida na kuonesha hasara kwa Kampuni ya TANCOAL ENERGY LTD, hivyo Serikali haikuweza kupokea gawio wala kukusanya kodi.

### 7.1.2 Gharama ya Kiasi cha Shilingi Milioni 940.34 na USD bilioni 3.35 zililipwa na TANCOAL Energy Ltd kwa Shughuli Zisizohusiana na Kampuni

Ukaguzi ulibaini kuwa TANCOAL ENERGY LTD imetumia kiasi cha Shilingi milioni 940.34 ambazo hazihusiani moja kwa moja na uchimbaji wa madini na shughuli nyingine za Mgodi kwa mujibu wa makubaliano ya Ubia.

Kadhalika, uchambuzi umeonesha kuwa, jumla ya Dola za Marekani bilioni 3.35 zililipwa kwa TANCOAL ENERGY LTD nchini Malawi (Kampuni Tanzu ya Intra Energy) kama gharama za shughuli za madini ikiwa ni pamoja na ada ya ushauri, gharama za usafirishaji, kukodisha mtambo, masoko, uhamisho wa fedha kwenda Intra Energy Malawi. Hata hivyo, malipo yote hayakuhusiana na shughuli za TANCOAL ENERGY LTD.

Matumizi haya yamesababisha TANCOAL Energy Ltd kutoripoti faida, hivyo, Serikali haikuweza kupokea gawio wala kukusanya kodi.

**Mapendekezo:**

Ninaishauri Serikali:

1. Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kuchukua hatua za kinidhamu na za kisheria kwa maafisa walioshindwa kutimiza majukumu yao kwa ufanisi, na hivyo kusababisha hasara kwa fedha za wanachama.
2. Kuhakikisha kuwa uwekezaji ulioanzishwa wa MCBL na Mwalimu House unaendeshwa vizuri kupitia sera iliyowekwa ya uwekezaji ambayo itaweka malengo na njia za kufikia malengo yaliyopangwa.
3. Kuhakikisha makusanyo ya mapato ya jumla ya Shilingi 205,466,447 na Shilingi 132,365,604 zilizoongezwa kwenye ununuzi wa kiwanja kwa udanganyifu, Kasumulu Kyela, Mbeya zinarejeshwa na kuwekwa kwenye akaunti ya Serikali;
4. Ihakikishe urejeshwaji wa jumla ya Shilingi Milioni 402.21 kutoka Kampuni ya BMTL (sasa The Copy Cat Tanzania Ltd).
5. Kuhakikisha urejeshwaji wa kiasi cha jumla ya Shilingi milioni 167.44 kutoka kwa Gotham International Limited na hatua stahiki zichukuliwe na Mamlaka ili kuhakikisha uzingatiwaji wa mikataba katika malipo ili kuepusha hasara zisizotarajiwa.
6. Ihakikishe kuwa Gotham International Limited inarejesha jumla ya kiasi cha Dola za Marekani 551,500 zilizolipwa kwa ajili ya kufanya mapitio ya sheria ambayo hakuifanya.
7. Kutekeleza mapendekezo kama yalivyoainishwa katika ripoti ya ukaguzi maalumu wa soko la Mwanjelwa.
8. Kuimarisha usimamizi katika uendeshaji wa ubia ili kuhakikisha kuwa ripoti zote za fedha ni sahihi.

9. Kuhakikisha kuwa malipo yote yasiyofaa na kiasi kilichopatikana na TANCOAL Energy Ltd kinarejeshwa tena na kurejea taarifa zao za kifedha kwa kuondoa malipo yasiyo ya lazima.

## SEHEMU YA SABA

## 7. Ripoti ya Ujumla ya Ukaguzi wa Ufanisi

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Katika ukaguzi wa ufanisi ofisi yangu imeandaa ripoti ya ujumla na ripoti zingine kumi zinazogusa maeneo mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli za serikali. Ripoti ya ujumla imelenga uchambuzi wa masuala ya usalama wakati ripoti zingine zimelenga maeneo ya ukaguzi ambayo ofisi yangu iliyapa kipaumbele katika mpango kazi wake kwa mwaka wa fedha 2017/18. Ufuatao ni muhtasari wa ripoti hizo:

Ripoti imetoa uchambuzi wa masuala ya usalama katika eneo la usafirishaji, ubora wa chakula na katika makazi ya watu. Uchambuzi huu umebaini yafuatayo:

### 7.1 Usalama katika Usafirishaji

- Usimamizi duni katika uwekaji wa alama za barabarani, michoro na kingo za barabara. Pia, kutokukarabati samani chakavu za usalama barabarani.
- Ukaguzi wa meli ndogo haukufanyika ipasavyo. Ilibainishwa kuwa asilimia 85 ya meli ndogo hazikufanyiwa ukaguzi ili kuona kama ni salama kwa kusafirishia abiria na mizigo.
- Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini haikuhuisha kanzidata ya meli ndogo na kusababisha kukosekana na taarifa muhimu za meli.
- Kutochukua hatua stahiki kwa ukiukwaji wa sheria za usalama. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 na 2015/2016 asilimia 2 tu ya wakiukaji wa Sheria ya Usafiri Majini walichukuliwa hatua.
- Alama za barabarani kwa watu wenye ulemavu kutokuwa toshelevu katika maeneo ya mijini na vijijini. Licha ya TANROADS kupanga kuweka alama 718 kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa mwaka 2015/2016 katika mikoa nane iliyotembelewa; ni asilimia 15 tu ya alama hizo ziliwekwa.

### 7.2 Usalama wa ubora wa chakula

- Ukaguzi ulibaini uwepo wa uwiano mkubwa wa kazi kwa mkaguzi mmoja wa ubora wa chakula ambao ulikua kati ya tani za mizigo 22,000 mpaka 1,476,000 kwa mwaka. Kiuhalisia ni vigumu kwa mkaguzi kukagua mizigo yote hiyo kwa ufanisi, jambo linalohitaji uwepo wa ukaguzi unaozingatia viashiria hatarishi. Hatahivyo, ni asilimia 10 tu ya wakaguzi katika ofisi za kanda za TFDA na

maeneo ya mipakani (waliohojiwa) walikua wamepata mafunzo ya namna ya kufanya ukaguzi unaozingatia viashiria hatarishi.

- Upungufu wa wakaguzi wa ubora wa nyama. Mfano katika machinjio ya vingunguti kulikuwa na upungufu wa asilimia 40. Wastani wa wanyama 100 hadi 150 kwa siku walikaguliwa na mkaguzi mmoja hali iliyoathiri ufanisi na usahihi wa ukaguzi.
- Asilimia 75 ya machinjio hayakuendeshwa katika mazingira ya usafi na usalama wa nyama na asilimia 67 ya nyama ilisafirishwa na magari machafu, yenye kutu na yasiyo na vibali vya kusafirisha nyama.

## 7.3 Usalama katika makazi ya watu

- Ukaguzi ulibaini Majengo mengi ya umma kuwa si salama dhidi ya moto kutokana na kutokuwa na viwango na vigezo vilivyohitajika kwa usalama dhidi ya moto.
- Utekelezaji duni wa hatua za usalama dhidi ya hatari ya moto katika majengo ya Umma. Majengo mengi yanayotumiwa na umma yako katika hatari kutokana na utekelezaji hafifu wa mahitaji ya usalama dhidi ya moto.
- Kikosi cha Zima Moto na Uokoaji hakikuwa na mpango madhubuti wa kukagua na kufuatilia shughuli za kuhakikisha majengo yote ya umma yanakaguliwa kwa ubora wa juu.
- Utekelezaji wa miradi ya maendeleo haukuwa rafiki kwa usalama wa makazi ya watu. Katika kipindi cha miaka mitano, jumla ya vibali vya ujenzi 17,692 vilitolewa ambapo miradi 24 tu ilikuwa imefanyiwa tathmini ya athari za mazingira.
- Baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokubalika kutekelezwa imekuwa vyanzo vya mafuriko na uchafuzi wa mazingira hali iliyohatarisha usalama wa binadamu. Mfano, ujenzi wa ofisi za Mradi wa Mabasi yaendayo haraka pale Jangwani.
- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais TAMISEMI haijaweza kudhibiti matumizi ya ardhi kwa sababu kuna miji mingi ambayo haijajengwa kiutaratibu kwa sababu ya ukosefu wa mpango kabambe wa mipango-miji.Katika mji uliopangiliwa, maeneo mengi ya wazi hayajasajiliwa na utekelezaji wake ni kinyume na mipango iliyowekwa. Kwa mfano, matumizi ya ardhi yalibadilishwa kutoka maeneo ya viwanda na kuwa makazi ya watu au kiunyume chake.

### 7.4 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi Yaliyotolewa Mwaka 2014

Ripoti hii ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi yaliyotolewa hapo awali inahusisha Ripoti Sita (6) za Kaguzi za Ufanisi kama zinavyoonekana kwenye Jedwali 1 zilizowasilishwa Bungeni katika kipindi cha mwaka 2014.

Jedwali Namba 1 linaonesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa yakiainishwa kama "***yametekelezwa kikamilifu***, ***yametekelezwa kwa kiasi***, ***hayakutekelezwa***, na yale ambayo ***yamepitwa na wakati kutokana na mabadiliko***"

**Jedwali Na. 6:** Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi

| Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi | Mapendekezo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla Kuu | Yaliyo tekelezwa Kikamilifu | Yaliyo tekelez wa Kiasi | Yasiyo tekelez wa | Yaliyopitw a na wakati |
| Usimamizi wa Udhibiti wa Gharama za Manunuzi Serikalini | 46 | 3 | 9 | 28 | 6 |
| Usimamizi wa ubora wa Chakula | 14 | 0 | 11 | 3 | 0 |
| Usimamizi Taka za Afya | 16 | 6 | 9 | 1 | 0 |
| Usimamizi wa kaguzi za Bidhaa zinazoingizwa nchini | 10 | 3 | 4 | 3 | 0 |
| Usimamizi wa Watoto Waishio katika Mazingira Hatarishi | 17 | 6 | 8 | 3 | 0 |
| Usimamizi wa Wanyamapori kwenye maeneo Tengefu | 18 | 13 | 3 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **121** | **31** | **44** | **40** | **6** |
| **Asilimia** | **100** | **26** | **36** | **33** | **5** |

Kwa ujumla, utekelezaji wa mapendekezo niliyotoa hauridhishi hususani ikizingatiwa kuwa ni asilimia 26 tu ya mapendekezo hayo yametekelezwa kikamilifu. Sehemu iliyobaki ya mapendekezo hayo ama hayajatekelezwa kabisa au utekelezaji wake bado unaendelea ingawa hadi sasa ni miaka 3 tangu mapendekezo hayo yatolewe.

Utekelezaji umekuwa si wa kuridhisha kutokana na taasisi za umma kutokuwa na mfumo madhubuti wa usimamizi wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za ufanisi.

### 7.5 Usimamizi wa Viuatilifu vya Kilimo

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini kama Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Maendeleo ya Mimea na Taasisi ya Utafiti wa Viuatailifu vya Kitropiki (TPRI) wanasimamia kwa ufasaha ubora wa viuatilifu vinavyoingizwa na kutengenezwa nchini

ili kuweza kulinda afya za watumiaji wa viuatilifu na mazingira kuhakikisha ardhi inaendelea kubaki katika ubora wake wa kuzalisha. Ukaguzi ulibaini yafuatayo:

- Uwepo wa viuatilifu visivyokidhi viwango na visivyosajiliwa katika mikoa yote ya Tanzania. Kwa kipindi cha mwaka 2013/14 jumla ya tani 1059 za viuatilifu vilivyopigwa marufuku viliingizwa nchini. Viuatilifu kama vile Abamite, Doom, Boss, Lava, Lethal, and Romectin vimekutwa vikiuzwa katika maduka na kutumiwa na wakulima pasipo kusajiliwa na TPRI.

- Ni asilimia 30 tu ya vituo vilivyopo mipakani vinavyoingiza viuatilifu nchini vimesajiliwa kudhibiti uingizaji

- Ukosefu wa miongozo ya ukaguzi unaotakiwa kufanyika kwa wauzaji wa pembejeo na kwenye mipaka ya kuingia nchini. Hii imesababisha mapungufu katika ukaguzi.

- Asilimia 80 ya wauzaji wa viuatilifu hawakuwahi kukaguliwa kabisa toka waanze kuuza viuatilifu vya kilimo takriban miaka 15 iliyopita. Vivyo hivyo, asilimia 67 ya wakaguzi wa viuatilifu hawakuwa na ujuzi wa kutosha kufanya ukaguzi na hivyo kufanya ukaguzi unaofanyika kutokidhi viwango.

Kulingana na mapungufu haya ni dhahiri kwamba wakulima hutumia viuatilifu visivyokidhi viwango na hivyo kusababisha, madhara kwa afya zao, mazingira na kupunguza uzalishaji wa kilimo, ukizingatia kwamba asilimia 81 ya watanzania wanategemea kilimo.

## 7.6 Usimamizi wa Ugawaji wa Viwanja

Ukaguzi ulilenga kutathmini kama Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia mamlaka ya Serikali za Mitaa wanasimamia kikamilifu ugawaji wa viwanja ili kuwezesha upatikanaji wa viwanja vya kutosha kwa gharama nafuu kwa ajili ya uendelezaji wa makazi nchini. Ukaguzi ulibaini yafuatayo:

- Mahitaji ya viwanja kwa nchi nzima yanakadiriwa kuwa viwanja 225,000 kwa mwaka wakati mamlaka za upangaji zilikuwa na uwezo wa kuzalisha wastani wa viwanja 132,201 kwa mwaka sawa na asilimia 59. Hii ilitokana na Mamlaka za Upangaji (Halmashauri) kukabiliwa na changamoto ya kupata ardhi iliyoambatana na gharama kubwa ya fidia na hivyo kufanya gharama za viwanja zisiwe nafuu.
- Zaidi ya asilimia 90 ya viwanja vilivyogawiwa havikuendelezwa ndani ya muda uliopangwa wa miezi 36.

- Asilimia 88 ya halmashauri zilizotembelewa hazikuwa na mpango kabambe kutokana na ukosefu wa wataalam jambo lililosababisha halmashauri kukosa mipango endelevu ya kukidhi mahitaji ya viwanja kwa siku zijazo.
- Kutokuwepo kwa mfumo shirikishi kati ya Wizara ya Ardhi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Halmashauri, na watoa huduma za miundombinu. Miradi yote mitano iliyotembelewa katika halmashauri zote nane haikuwa na miundombinu muhimu kutokana na kukosekana kwa mfumo huo.

## 7.7 Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Maji Taka maeneo ya Mijini

Lengo la ukaguzi lilikuwa kutathmini endapo utoaji wa huduma za maji taka katika maeneo ya mijini unaotekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zinasimamiwa ipasavyo ili kuzuia kuenea kwa magonjwa yanayohusiana na uchafuzi wa mazingira katika jamii. Ukaguzi ulibaini yafuatayo:

- Wastani wa asilimia 6 tu ya wakazi waishio mijini wanapata huduma kwa mtandao wa maji taka hadi mwaka 2016/17 ambapo ni chini ya lengo la MKUKUTA II la asilimia 22 kufikia mwaka 2015.

- Wastani wa asilimia 52 ya idadi ya watu waliopitiwa na mtandao wa maji taka katika Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira zilizokaguliwa, hawajaunganishwa kwenye mtandao huo. Matokeo yake, watu hutumia njia zisizofaa za uondoaji wa maji taka kama vile; kuyamwaga kwenye mito na mitaro hasa wakati wa msimu wa mvua kunakosababisha hatari ya kuenea kwa magonjwa ya mlipuko yatokanayo na uchafuzi wa mazingira.

- Kwa wastani katika mita za ujazo milioni 14.6 za maji taka zinazozalishwa kila mwaka katika miji iliyotembelewa, ni mita za ujazo milioni 1.3 tu (sawa na asilimia 9) zinazo kusanywa kupitia mfumo wa maji taka na kwa kutumia magari ya maji taka. Sababu kubwa ni uwepo wa mitandao chakavu ya maji taka isiyokidhi mahitaji halisi na ukosefu wa miundombinu ya ukusanyaji wa maji taka kwa wale wasiopitiwa na mtandao.

- Mitandao ya maji taka kutofanya kazi kwa kiwango kinachoridhisha. Katika mamlaka 3 kati ya 7 zilizotembelewa ambazo ni Tanga, Dar es Salaam na Dodoma, wakaguzi walibaini kuwa kuna utiririshaji na uzibaji wa mara kwa mara wa mitandao ya majitaka unaosababishwa na uduni wa ukarabati na uchakavu wa mitandao hiyo ambayo mingi ilijengwa kati ya miaka ya 1930 na 1980.

- Hali ya mabwawa ya kutibu maji taka hairidhishi hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa mfano, mabwawa ya Vingunguti and Kurasini yamejaa maji taka na yanaonekana kama kizimba cha kutupia taka ngumu. Hii inasababisha kazi ya uchujaji wa majitaka unaofanywa na mabwawa haya kuwa dhaifu licha ya kuwa DAWASCO wanakusanya pesa nyingi kutoka kwa wateja wanaokuja kumwaga majitaka kwenye mabwawa haya kwa njia ya magari.

## 7.8 Utoaji wa Huduma za kusaidia viwanda vidogo na vya kati nchini

Ukaguzi ulilenga kutathmini kama shughuli za utoaji huduma kwa wenye viwanda vidogo na vya kati zinawezesha ukuaji endelevu wa sekta ya viwanda vidogo na vya kati. Ukaguzi ulibaini yafuatayo:

- Sekta ya Viwanda vidogo na vya kati hivi sasa inakua kwa kiwango cha asilimia 5.6 wakati kasi ya kufunga biashara zao ni asilimia 8 licha ya uwepo wa ongezeko la jumla la idadi ya wajasiriamali kwa mwaka.
- Mchango wa sekta hii katika ajira nchini ni asilimia 40 kiwango ambacho ni chini ya malengo ya Wizara (cha asilimia 60). Pia Mchango wa sekta kwa pato la Taifa unakadiriwa kuwa ni asilimia 35, ambacho ni kiwango cha chini ya malengo ya Wizara (asilimia 40). Hii ilitokana na:

    - Utoaji Hafifu wa Huduma kwa wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati: SIDO imeweza kufikia Wajasiriamali na Wenye Viwanda Vidogo na vya Kati kwa kiwango cha asilimia 7 tu kulingana na kanzidata ya SIDO; na ni sawa na asilimia 0.4 ya makadirio ya Wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati waliopo nchini.
    - Michakato ya kibajeti ya Wizara ya Viwanda na SIDO haikutoa kipaumbele cha kutosha kwa kutenga fedha kwa shughuli za kuendeleza Wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati. Hii ilikwamisha utelezaji wa utoaji huduma katika sekta hii.

- Ufuatiliaji hafifu wa huduma zinazotolewa. Wizara imeweza kufanya asilimia 25 ya shughuli za ufuatiliaji, na SIDO iliweza kufanya asilimia 36 ya ufuatiliaji uliopangwa.

## 7.9 Usimamizi wa Taka za Kieletroniki

Lengo la ukaguzi huu lilikuwa kutathimini kama Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Muungano na Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeweza kusimamia kwa ufanisi ukusanyaji, usafirishaji na uteketezaji wa taka za kieletroniki nchini.

- Ukaguzi ulibaini kutokuwepo mikakati madhubuti ya kupunguza taka za kielektroniki nchini.Ndani ya miaka mitano (2013-2017) kulikuwa na tani 11,414 za taka za kieletroniki katika majiji yote nchini. Taka hizi zinajumuisha simu, kompyuta, vinakilishi, televisheni, redio na vifaa vya umeme. Serikali haikuweka mikakati yenye kulenga kupunguza uzalishwaji wa taka za kielektroniki nchini. Hakuwa na udhibiti imara kuhakikisha kuwa taka za kielektroniki zinakusanywa, zinahifadhiwa, zinasafirishwa na kuteketezwa ipasavyo.

- Pamoja na Baraza la Taifa la Kusimamia Mazingira kuingia mkataba wa Jumuia ya Afrika Mashariki wa kuhakikisha madhara taka za kieletroniki yanapungua ifikapo 2030 lakini hapukuwepo na mkakati wala bajeti ya kuweza kufikia lengo kusudiwa.

- Ukaguzi ulibaini kuwa serikali haikuwa na mpango mikakati ya uelimishaji na ujengaji uwezo juu ya udhibiti wa taka za kieletroniki kwa umma na sekta binafsi. Kwa mfano, kati ya mwaka 2014/2015 mpaka 2016/2017, Baraza la Taifa la Usimamizi wa mazingira lilitengewa Tsh 53 millioni kwa ajili ya kuandaa na kusambaza vipeperushi **26,800** na kusambaza vipeperushi **3600** sawa na asilimia **13** vilisambazwa kwa ajili ya siku za sikukuu za wakulima na siku ya mazingira duniani zilizofanyika katika ofisi za kanda za Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira. Usambazaji huo wa vipeperushi haukupangiliwa na pia vipeperushi hivi pia havikuwa na taarifa za masuala ya usimamizi wa taka za kielektroniki.

- Pia mwaka 2016/2017, Baraza la Taifa la Mazingira lilitumia Tsh 46 millioni kwa ajili ya kuandaa vipeperushi vya uelimishaji juu ya mazingira 23,000 ambavyo kabla ya kukamilisha usambazaji serikali ilibadilisha uamuzi na kuruhusu matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo pia taarifa zake zilikuwemo katika vipeperushi hivi. Hii ilisababisha kutosambazwa kwa vipeperushi 22,600 na kusababisha hasara kwa serikali.

- Pia wadau 58 wa sekta binafsi walisajiliwa na Baraza la Taifa la Mazingira kati ya mwaka 2012 hadi 2016 kwa ajili ya kukusanya, kusafirisha, kuchakata na kuteketeza vyuma chakavu, lakini hakukuwa na ushirikishwaji juu ya usajili wao baina ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na Halmashauri za Serikali za Mitaa. Kutokaguliwa kwa wafanyabiashara hawa wa taka za kielektroniki ilisababisha ongezeko la wafanya biashara wasio kuwa na vibali vya ukusanyaji, kuhifadhi na usafirishaji wa taka za kielekronikin. Ongezeko hili la wafanyabiashara wasiosajiliwa lilichangiwa pia na ongezeko la ada za usajili ambazo zilipandishwa kutoka Tsh 600,000 mpaka Tsh 10 millioni.

## 7.10 Usimamizi wa Maeneo Tengefu ya Ukanda wa Pwani

Lengo la ukaguzi huu ilikuwa ni kutathmini kama Kitengo cha Hifadhi za Bahari (MPRU) kinafanya udhibiti na uhifadhi endelevu wa rasilimali za bahari katika maeneo tengefu kama invyohitajika. Ukaguzi huu ulibaini kuwa:

- Kitengo cha Hifadhi za Bahari hakijaweza kudhibiti ipasavyo matumizi ya rasilimali katika maeneo tengefu kwa kutumia mifumo yake ya utoaji wa vibali. Aidha, MPRU haijafanya ufuatiliaji wa kuridhisha wa rasilimali za baharini. Mbali na hilo, MPRU haijafanikiwa ipasavyo kuratibu na kuhusisha wadau katika ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za baharini.

- Kwa mfano, hifadhi za bahari za Tanga na Mtwara hazikuzingatia kanuni za utoaji wa vibali vya matumizi ya rasilimali kwa wakazi na utaratibu wa kuwapa vibali vya matumizi ya rasilimali kwa watu wasio wakazi wa ndani ya hifadhi haukufuatwa. Shughuli mbalimbali za uwekezaji kama vile hoteli na visima vya gesi asilia vilivyoko ndani ya maeneo ya hifadhi havijafanyiwa tathmini ya kimazingira ili kubaini athari ambazo zinaweza kusababishwa na shughuli hizo kwa mazingira ya bahari. Kati ya miradi mbalimbali ya uwekezaji inayozidi 54 katika hifadhi zote, ni mradi mmoja tu (wa hoteli huko Shungimbili), Mafia ambao ulipitia mchakato wa tathimini ya mazingira

- Ukaguzi ulibaini kuwa zaidi ya wavuvi 240 wamevamia kinyume na sheria kisiwa cha Nyororo ambacho kiko ndani ya eneo la hifadhi. Pamoja na juhudi za kuwazuia kufanya shughuli hizi, halmashauri ya Wilaya ya Mafia imeendelea kutoa leseni za uvuvi kwa wavuvi wasio halali ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa.

- Ukaguzi pia ulibaini kuwa shughuli za doria katika maeneo ya ulinzi wa bahari hazifanyiki za kutosha.Hifadhi ya bahari ya Mafia tu ndio imekuwa ikifika lengo

la utekelezaji wa doria lakini Hifadhi zingine kama Tanga, Mtwara na Dar es Salam doria zimefanyika kwa kiwango cha asilimia 11 hadi 44 tu.

- Ukaguzi huo umeonyesha kwamba zaidi ya 90% ya doria hazikuwa na ushiriki wa kamati za hifadhi na mahusiano za vijiji. Kamati za Uhusiano uhifadhi za vijiji hazikuanzishwa katika vijiji vyote ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa wakati wa ukaguzi. Kamati hizi husimamia uhifadhi katika ngazi ya kijiji hazikuhusika vya kutosha katika shughuli za doria katika hifadhi ya Bahari.

### 7.11 Usimamizi wa Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu Ya Juu

Lengo la ukaguzi kuu ilikuwa ni kubaini jinsi gani Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imendaa na kutekeleza mikakati ya urejeshwaji wa mikopo toka kwa wanufaika. Pia Ukaguzi ulitahimini jinsi gani Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia inavyosimamia utendaji wa Bodi hii.

- Ukaguzi ulibaini Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu haikuweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa mikopo iliyojiwekea kwa kipindi cha miaka sita ya fedha 2011/12 hadi 2014-2017 ambayo ilikuwa ni kukusanya mikopo angalau kwa asilimia 70 na 80 ya mikopo yote iliyoiva. Hata hivyo ukaguzi ulibaini kuwa ukusanyaji mikopo katika kipindi hiki kwa wastani ulikuwa ni kati ya asilimia 32 na 48 tu ya mikopo yote iliyoiva.

- Hata hivyo ukaguzi ulibaini kuwa taarifa za makusanyo kwa kulinganisha miaka ya sasa na ile ya nyuma yaliongezeka. Kwa mfano makusanyo yaliongezeka toka toka TZS 28 mpaka 116 bilioni kwa mwaka 2015/2016 and 2016/2017 ukulinganisha na kipindi cha nyuma (2012/2013-2014/2015) ambapo makusanyo yalikuwa kati ya TZS 15 na 22 bilioni.Mbali na jitahada hizi za menejimenti iliyopo bado malengo ya ukusanayaji mikopo hayakufikiwa.

- Sababu za kutofikiwa kwa malengo ni kutokuepo kwa mikakati madhubuti na usimamizi wa kutosheleza wa shughuli zinazohusiana na urejeshwaji wa mikopo hii.Mfano kanzidata ya mikopo haikutumika kikamilifu katika kupanga utekelezaji wa kubaini wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu. Pia uandaaji duni wa mikakati ya kubaini wanufaika wa mikopo na njia za ukusanyaji ikiwemo kutoa ankara kwa wakati kwa wanufaika wa mikopo hii ziliathiri ukusanyiji wa mikopo hii.

- Ukaguzi pia ulibaini Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikusimamia utendaji wa Bodi ya Mikopo katika suala la urejeshaji wa mikopo ipasavyo. Wizara ilijikita zaidi katika kufuatialia utoaji wa mikopo kwa wanufaika na kuweka jitahada hafifu katika kusimamia utendaji wa Bodi katika kutekeleza

shughuli za urejeshwaji wa mikopo. Hii ilitokana na Wizara kukosa mbinu mkakati wa kukafuatilia na kutahmini utendaji wa Bodi ya Mikopo. Kwa mfano katika wanufaika wa mikopo 163,394 waliokiuka masharti ya urejeshwaji wa mikopo hii, ni wanufaika wawili tu ndio waliofikishwa mahakamani.

### 7.12 Maandalizi ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)

Lengo la ukaguzi huu ni kutathmini jinsi gani nchi imejiandaa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu.

- Ukaguzi huu ulibaini kuwepo kwa mapungufu katika ujumuishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika mipango ya maendeleo ya nchi. Hakukuwa na mikakati madhubuti ya kujengea umma uelewa juu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kuanzia ngazi ya kitaifa hadi ngazi ya jamii; ushirikishaji mdogo wa wadau; na mfumo dhaifu wa kitaasisi kwa ajili ya kujumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu katika mipango mikakati ya kitaifa.

- Wizara ya Fedha na Mipango haijabainisha kikamilifu rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Pamoja na kwamba asilimia 68 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yamejumuishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo, asilimia 87 ya fedha zilizokadiriwa zimeelekezwa katika miradi ya vielelezo (flagship projects) ambayo ni sehemu tu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu katika upande wa kiuchumi. Masuala ya mazingira na kijamii hayakuzingatiwa kikamilifu katika mgao wa rasilimali hizi. Aidha njia mpya zilizobuniwa kwa ajili ya ukusanyaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu hazitoshelezi na nyingine kama dhamana za mitaji kutoka manispaa na serikali za mitaa hazitekelezeki.

- Licha ya mapato yatokanayo na kodi kuwa asilimia 68 ya mapato ya ndani, wigo wa kodi (tax base) ni mdogo kutokana na kwamba Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mamlaka ya Mapato haijaweka kanzidata ya kuwatambua walipa kodi wote hasa wale wasio katika sekta rasmi. Pia hakuna mikakati rasmi ya kuwafuatilia walipa kodi wasio na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN).

- Pia Wizara ya Fedha na Mipango haijaweka mfumo madhubuti na jumuishi kwa ajili ya ufuatiliaji, tathmini, mapitio na utoaji taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu baina ya sekta.

## 7.13 Hali ya Uharibifu wa Ardhi, Misitu na Ukataji Miti

Lengo la utafiti huu ni kutathmini kiwango cha hali ya uharibifu wa ardhi, misitu na ukataji miti nchini.

- Kiasi cha wastani wa hekta 236,711.2 za misitu kwa mwaka hupotea katika halmashauri 48 zilizoangaliwa katika tathmini hii. Tathmini hii pia imeonyesha, uchomaji wa misitu, kilimo na ufugaji usio endelevu pamoja na utekelezaji hafifu wa sheria umesababisha uharibifu mkubwa wa msitu. Madhara makubwa yaliyo bainishwa na tathmini hii, ni yale yanayo husiana na hasara za kiuchumi, mmomonyoko wa ardhi, ukame, mafuriko na ongezeko la migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

- Kwa upande mwingine, uharibifu wa ardhi kwa sehemu kubwa umesababishwa na matumizi mabaya ya ardhi, ufugaji na kilimo kisicho endelevu, mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la watu. Kwa ujumla, tathmini ilionyesha kwamba kiwango cha uharibifu wa ardhi nchini ni cha wastani. Kwa nchi nzima, matumizi mabaya ya ardhi ndio chanzo kilichoongoza katika kusababisha uharibifu wa ardhi. Sababu nyingine ni pamoja na uchimbaji holela wa madini na ukosefu wa miundombinu ya mifugo. Halmashauri tano kati ya 48 zilionyesha kuna uharibifu mkubwa sana wa ardhi. Madhara ya uharibifu wa ardhi ni pamoja na mmomonyoko wa udongo, upungufu wa rutuba ya udongo na ongezeko la madini chumvi katika udongo ambapo hupelekea athari katika uzalishaji wa chakula.

**Mapendekezo**

(i) Ninapendekeza Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha wizara na mamlaka au wakala zinazowajibika kuhakikishia usalama katika maeneo matatu ambayo ni uchukuzi, ubora wa chakula na makazi ya watu zinaandaa na kutekeleza dhana ya mbinu msingi ya viashiria hatarishi katika kupanga na kufanya kaguzi zinazohusiana na usalama. Pia kuhakikisha Wizara, mamlaka au wakala hizi zinakuwa na viashiria muhimu vya kupima utendaji ili kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mikakati yao.

(ii) Ninapendekeza Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kuwa Wizara, Idara, Wakala pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweka kipaumbele katika ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi, ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za ufanisi.

(iii) Ninapendekeza Wizara ya Kilimo kuwa na usimamizi madhubuti wa viuatilifu; mipango ya ukaguzi wa viuatilifu ijumuishe maeneo hatarishi; kuwa na mfumo wa uratibu utakaohakikisha taasisi za serikali ambazo ni watekelezaji wa shughuli za viuatilifu wanafanya kazi kwa pamoja.

(iv) Ninapendekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia mamlaka ya Serikali za Mitaa waboreshe usimamizi wa shughuli za ugawaji wa viwanja ili kuwezesha upatikanaji wa viwanja vya kutosha vyenye miundombinu muhimu na kwa gharama nafuu.

(v) Ninapendekeza Wizara ya Maji ihakikishe kuwa mamlaka zote za Maji Safi na Usafi wa Mazingira zinatengeneza mpango wa jumla kwa ajili ya kutoa huduma ya majitaka, ikiwa ni pamoja na kutenga rasilimali fedha.

(vi) Pia, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihakikishe kuwa Halmashauri zote zinaandaa mpango wa kati na wa muda mrefu wa utoaji wa huduma za maji taka kwenye maeneo ya miji ambayo hayajafikiwa na mitandao ya maji taka.

(vii) Ninapendekeza Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itengeneze mfumo endelevu wa kuzipatia fedha shughuli za maendeleo katika sekta ya wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati. Pia itengeneze mfumo wa ukuasanyaji wa taarifa muhimu za kuwezesha kufahamu idadi, mahitaji halisi ya Wenye Viwanda Vidogo na Ukuaji wa sekta hii kwa ujumla.

(viii) Ninapendekeza Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Raisi Mazingira na OR - TAMISEMI inatakiwa kuhakikisha Baraza la Taifa la Mazingira pamoja na halmashauri za serikali za mitaa zinajengewa uwezo madhubuti wa kusimamia taka za kielektroniki. Pia serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais irasimishe Miongozo ya usimamizi wa taka za kielektroniki na kuhakikisha wadau wote wanapatiwa na kuzitumia ili kupunguza na kusimamia kwa ufanisi shughuli zinazohusiana na taka za kielektroniki.

(ix) Ninapendekeza MPRU kuanzisha mfumo ambao utaunganisha maelezo ya waombaji wa leseni na taarifa zilizopo katika kamati za hifadhi za vijiji. Pia, waimarishe mifumo ya kudhibiti shughuli za uwekezaji zilizopo ndani ya hifadhi na kuhakikisha kuwa shughuli zao zinazingatia kanuni za mazingira. Zaidi ya hayo MPRU inapaswa kuweka Viashiria vya Utendaji muhimu ili kuwezesha tathmini ya utendaji wa hali ya rasilimali za baharini na hatimaye kunzisha mwongozo wa mamna ya kutathmini manufaa ya fursa za kiuchumi zinazojitokeza ili kuamua kama zinaendana sambamba na malengo ya uhifadhi wa rasilimali za bahari.

(x) Ninapendekeza Ofisi ya Makamu wa Rais, na Wizara za kisekta ziratibu uandaaji wa mikakati endelevu ya kupunguza matumizi yasiyofaa ya ardhi na misitu; Kubuni mikakati kwa kushirikiana na Wizara ya elimu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa katika kutoa elimu ya mazingira; Kusimamia sera ya

kudhibiti ufugaji holela na kuratibu na kuunga mkono jitihada mbalimbali za kuhifadhi mazingira .

(xi) Halikadhalila, Wizara ya Maliasili na utalii ihahakishe inaweka alama na mipaka madhubuti katika misitu ya hifadhi na maeneo ambayo yako chini ya Mamlaka ya Huduma za Misitu; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa (TAMISEMI) ihakikishe kuwepo kwa mbinu mbalimbali za kudhibiti shughuli za kimaendeleo katika maeneo ya hifadhi za misitu; kusimamia uanzishwaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika kila halmashauri.

(xii) Ninapendekeza Bodi ya Mikopo kuwa na mikakati madhubuti yenye malengo yanayopimika. Pia Bodi inatakiwa kuboresha kanzidata yake ya ukusanyaji wa mikopo na mifumo ya utoaji taarifa za mikopo ili zoezi la kubaini na kutoa ankara kwa wanufaika lifanyike kwa ufanisi. Wizara inapaswa kuandaa mkakati wa kupima na kufuatilia utendaji wa Bodi ya Mikopo hasa katika urejeshaji wa mikopo.

(xiii) Ninapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango iandae mkakati ambao utaongoza utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu sambamba na mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano.Pia wizara inapaswa kufanya tathmini ya jitihada za ukusanyaji rasilimali na kubainisha njia bunifu za kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi kwa ajili ya kuongeza rasilimali zinazohitajika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu.Kuanzisha mkakati uliojitosheleza katika kuratibu, kusimamia na kutoa taarifa za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**HITIMISHO**

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Masuala yaliyoainishwa kweye ripoti zilizowasilishwa Bungeni leo ni mengi na muhtasari huu unaainisha baadhi ya masuala hayo. Ni imani yangu kuwa mtapata muda wa kuzisoma kiundani ili muweze kuelimisha umma bila kuharibu maudhui ya ripoti hizi.

Aidha, ripoti hizi zinapatikana kupitia tovuti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayosomeka www.nao.go.tz na tovuti ya Bunge www.parliament.go.tz pamoja na tovuti ya Serikali www.tanzania.go.tz. Aidha, nakala laini zimeandaliwa na mtapewa kwa ajili ya kurahisisha kuhabarisha umma.

Pia, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kipaumbele alichokitoa wakati wa kupokea ripoti hizi, pamoja na Serikali nzima ya awamu ya tano kwa adhma yao ya kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa kupitia ripoti hizi. Shukrani hizi pia nazitoa kwa Wenyeviti wa Kamati za Bunge za Kudumu (PAC na LAAC na Kamati zingine zote za Bunge) kwa kuendelea kutumia ripoti hizi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru waandishi wa habari kwa kuendelea kuhakikisha kuwa masuala yaliyoainishwa katika ripoti hizi yanaifikia jamii kwa wakati na pale inapolazimu kupata ufafanuzi kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.



Prof. Mussa Juma Assad,

**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**